TANGAZO LA SERIKALI NA. 710 la tarehe 02/12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA UGANSA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Ugansa ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

“Unaanzia alama ya mpaka ya upimaji U1 katika makutano ya barabara ya Kigoma na Mchina yenye majira-nukta 316243E, 9441554N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kusini-Magharibi katika uelekeo wa S180$^{0}$12’0”W kwa umbali wa kilomita 1.8 hadi alama ya mpaka ya upimaji U2 yenye majira-nukta 315440E, 9439767N; baada ya hapo mpaka utaelekea Magharibi katika uelekeo wa W100$^{0}$6’40” kwa umbali wa kilomita 1.4 hadi alama ya mpaka upimaji U3 iliyopo barabara ya Usinge yenye majira-nukta 314047E, 9439707N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kaskazini hadi alama ya mpaka ya upimaji U4 iliyopo barabara ya Kigoma yenye majira-nukta 314000E, 9440350N; baada ya hapo mpaka utaendelea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa N170$^{0}$11’20”E kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi alama ya mpaka ya upimaji U5 yenye majira-nukta 314554E,

9442665N; baada ya hapo mpaka utapita Kaskazini mwa makazi ya Ugansa Mashariki-Kusini kutoka alama ya mpaka ya upimaji U5 katika uelekeo wa E95$^0$6’20”S kwa umbali wa kilomita 2.12 hadi alama ya mpaka ya upimaji U6 yenye majira-nukta 316674E, 9442551N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa S65$^0$4’20”W kwa umbali wa kilomita 1.7 hadi ulipoanzia”.

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*